**Jina**.................................................................**Nambari ya mtahiniwa**...................................
**Tarehe**.................................... **Darasa**..............................

**KIDATO CHA TATU**
**KISWAHILI**
**JARIBIO LA MWISHO WA MUHULA WA PILI 2026**
**MUDA:SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako, nambari yako na darasa katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

b) Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa.

c) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**KWA MATUMIZIYA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| A.UFAHAMU | **15** | |
| B.UFUPISHO | **15** | |
| C.LUGHA | **40** | |
| D.ISIMUJAMII | **10** | |
| E.FASIHI SIMULIZI | **20** | |
| **JUMLA** | **100** | |

**SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)**
**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Takwimu za hivi punde zinaonyesha kuwa maradhi ya saratani imejifaragua na kuwa miongoni mwa **senene kuduku** duniani maadam inatishia kuupiku ukimwi. Wagonjwa wanaoendelea kuyasalimia amri wanaelekea kufikia kiwango cha kutisha. Licha ya tawala nyingi duniani kuwekezea tafiti anuai za kuyapindua, miale ya welewa wa kiini chake bado ni hafifu ajabu. Wataalam wa utabibu wanaeleza chanzo cha saratani kama mgawanyiko usio wa kawaida wa chembechembe za damu katika viungo vya mwili vinavyohusika. Viungo huanza kukua kwa kasi isiyo ya kawaida.

Japo uvumbuzi unaonyesha kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa watu wa umri wa makamo kuambukizwa ugonjwa huu. Wazee wamo hatarini zaidi.Hata hivyo vimeshuhudiwa visa vingi ambavyo hata watoto wachanga huathiriwa pakubwa.Saratani ya tezi-kibofu, ya koromeo na ya mapafu ni baadhi ya aina zinazowaathiri wanaume. Saratani ya tezi-kibofu huwasogelea zaidi mabuda wa umri wa miaka zaidi ya sitini. Kwenda haja ndogo kila mara. Ugumu wa kupitisha mkojo, ugumu wa kuanza au kumaliza kukojoa, damu kwenye mkojo na maumivu ya mgongo ni baadhi ya dalili zake. Mwishowe, tezi-kibofu huzidi kuwa kubwa na kufungia mkojo kutoka.

Kansa zinazowalenga sana wanawake ni pamoja na ya nyumba ya uzazi, mlango wa uzazi na **maziwa**.Kansa ya maziwa huwachachawiza zaidi wanawake wenye umri wa miaka thelathini na mitano au zaidi. Dalili ya awali ni uvimbe unaohisika kwa ndani na maziwa kutoa usaha. Inaenea haraka na kuviambukiza viungo vya ujirani mathalani mapafu na ini. Saratani ya mlango wa uzazi inaambukizwa na virusi vinavyoita papolloma. Virusi hivi hupata mwanya iwapo mwanamke alianza mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo,akiwa na wapenzi wengi, akiwa katika matumizi ya dawa fulani za kupanga uzazi na apulizapo moshi wa sigara.

Inapendekezwa kuwa **ukaguzi wa ada** ufanywe ili kuugundua kabla haujasambaa kutokana na kauli kwamba mwanzoni hausababishi uchungu wowote. Ukaguzi wa kibinafsi kwenye viungo vilivyo na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa kisha jambo lolote lisilo la kawaida kama vile uvimbe na ugumu wa kumeza liwasilishwe mara moja kwa daktari. Ushauri zaidi unahusu aina ya vyakula na mitindo ya kisasa ya maisha. Vyakula vilivyosheheniwa na protini zipatikanazo katika nyama na mayai ni miongoni mwa vyakula hatari. Vyakula vya kiasili kama mboga, miwa, matunda, mafuta yanayotokana na mimea na nyama nyeupe hupendekezwa. Uvutaji wa sigara, unywaji pombe, na baadhi ya vipodozi vyenye zebaki huweza kurutubisha uwezekano wa kuambukizwa saratani.

Ijapokuwa saratani ni kama sikio la kufa lisilosikia dawa, ni muhimu wawele wazibe ufa kabla ya kuangukiwa na ukuta usioweza kujengeka tena. Ikigunduliwa mapema.Maradhi haya huweza kudenguliwa kutumia tibakemikali, tibamiale, chanjo dhidi ya baadhi ya virusi vya saratani, upasuaji wa viungo vilivyoathiriwa na dawa za kupunguza makali yake.

Utafiti wa kina uliofanywa na kukamilishwa mwezi wa Machi, mwaka wa 2014 na madktari wa Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta kwa ushirikiano wa wengine kutoka Uingereza umegundua kuwa dawa aina ya Lopinavir inayotumiwa kupunguza makali ya ukimwi ina uwezo wa kukabiliana na maradhi haya.

Uchunguzi uliofanyiwa wawele baada ya muda fulani wa uwekaji wa dawa hii kwenye mlango wa uzazi ulibainisha kuwa chembechembe za saratani huangamizwa na dawa hii. Ni jambo la kutia moyo kuwa harakati za kukabiliana na janga la ukimwi zinaelekea kutoa suluhu kwa maradhi haya ya kansa. Inakuwa shani inaposadifu kuwa nuhusi iliyowahi kutokea katika mapisi ya siha ya insi imekuwa kitivo kinachopaswa kuenziwa. Hakika hizi ni harakati zinazostahili kupongezwa na kuzidishwa iwapo zimwi hili litafukiwa katika lindi la usahaulivu.

a) Kwa nini maradhi ya saratani yanaelekea kuwa hatari zaidi kuliko ukimwi? (alama.1)
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………….…..

b) Ni kwa nini ni vigumu kuitambua saratani mwanzoni? (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………….

c) Taja mambo yanayoweza kuchangia maambukizi ya saratani ya mlango wa uzazi.(alama 3)

………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

d) Eleza njia ambazo mtu anaweza kutumia kugundua kama ana saratani. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………….

e) Eleza baadhi ya mambo yanayoweza kuchochea maambukizi ya saratani. (alama 2)
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

f) Eleza maana ya methali ifuatayo kwa mujibu wa makala haya. (alama.2)

Dalili ya mvua ni mawingu.

………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………..

g) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye makala. (alama 3)

i) senene kuduku…………………………………………………………………

ii) maziwa
………………………………………………………………………

iii) Ukaguzi wa ada……………………………………………………………..

**SEHEMU YA B: UFUPISHO (AL.15)**

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine.

Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema `maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti, kuyaendesha, kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: `Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine wengi pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia za ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano, kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano, neno `mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa `mjinga', `mjanja', `hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za ueneaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 55 - 60) (alama 5, 1 ya Mtiririko)

**Matayarisho**

………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.
(maneno 100-110) (alama 8, 1 ya Mtiririko
**matayarisho.**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi.**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

## SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Taja sauti zifuatazo. (ala 3)

i) Kipasuo hafifu cha kaakaa laini...................................................................

ii) Nazali ya kaakaa gumu.............................................................................

iii) Kikwamizo ghuna cha ufizi.........................................................................

b) Eleza miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-I.Toa mifano. (ala 2)

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
...........................................................................................................................

c) Ainisha vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (ala 2)

Kambazi angali barabarani na angali anaendesha baiskeli ambayo imechakaa.

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

d) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (ala 2)

Afaye

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
...................................................................

e) Tambua nyakati na hali katika sentensi ifuatayo.

Mhazigi atakuwa ameunganisha mifupa iliyovunjika. (ala 1)

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

f) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi hii.

Kwa nini umeishi kwao kwa miaka mingi? (ala 3)

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

g)Toa mfano mmoja wa kitenzi cha asili ya kigeni kisha ukinyambue katika kauli ya kutendesheka. (ala1)

..........................................................................................................................................

h) Tunga sentensi mbili ili kubainisha maana mbili za neno 'kiwavi'. (ala 2)

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................

i) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi tahini. (ala 2)

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................

j) Changanua kwa njia ya mishale. (ala 4)
Kikulacho ki nguoni mwako.

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
..............................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
..............................................................................................................................

k) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (ala 2)
Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano.

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................

l) Yakinisha sentensi ifuatayo . (ala 2)
Asipofika mapema hatampata.

.....................................................................................................................................................

m) Onyesha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo. (ala 3)
Mwiti alimbebea mjomba mzigo kwa baiskeli.

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................
..............................................................................................................................

n) Akifisha sentesi zifuatazo. (ala 2)
I) Mama sokoni ataenda asubuhi kesho.

.....................................................................................................................................................

ii) Gazeti la Taifa Leo huandikwa kwa Kiswahili.

.....................................................................................................................................................

o) Andika katika usemi halisi. (ala 3)
Chifu wetu alituambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu.

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................

p) Kanusha katika ukubwa. ( ala 3)
Mwizi huyu aliiba kisu na ng’ombe wa mwanamke yule.

.....................................................................................................................................................
.....................................................................................................................................................

q) Eleza tofauti iliyo kati ya sentensi hizi. ala 2)
i) Tulipofika hotelini tulipewa soda na chupa.

.....................................................................................................................................................

ii) Tulipofika hotelini tulipewa soda kwa chupa.

.....................................................................................................................................................

r) Andika neno lingine lenye maana sawa na; (ala 1)
Piku

.....................................................................................................................................................

**SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Kwa nini kulikuwa na haja ya **kusanifisha** lugha ya Kiswahili. Toa sababu **tano**. ala 5)

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………………

b) ……………..Sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa

i) Tambua **sajili** iliyotumika katika dondoo hili ala 1)

……………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

ii) Eleza **sifa nne** za sajili hiyo. ala 4)

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………………

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)**

a) Ni jukumu la jamii **kudumisha** Fasihi Simulizi. Dhihirisha. (alama 6)

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………

b) Huku ukitoa mifano, onyesha **udhaifu** wa miviga. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………

(c ) Taja aina **nne** za miviga ambayo hupatikana katika jamii ya kisasa. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………

(d ) Eleza **nafasi** ya miviga katika jamii. (alama 5)

…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………………
…..